**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

**SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA**

ISO 9001:2015 Certified

*Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali*

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU USAJILI NA UKAGUZI WA MAENEO YA BIASHARA YA BIDHAA ZA CHAKULA NA VIPODOZI

**Dar es Salaam, 25.02.2026**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ni taasisi ya umma ambayo pamoja na majukumu mengine husimamia ubora na usalama wa bidhaa za chakula na vipodozi kwa mujibu wa Sheria ya Viwango, Sura ya 130 na Kanuni zake ili kulinda afya za watumiaji. Katika kutekeleza jukumu hilo, Shirika husajili na kufanya ukaguzi wa maeneo ya uzalishaji, uhifadhi, usambazaji na uuzaji ili kuhakikisha kuwa bidhaa hizo zinakidhi matakwa ya ubora na usalama.

Usajili wa maeneo ya biashara yanayohusika na bidhaa za chakula na vipodozi hufanyika ili kuhakikisha kuwa maeneo hayo yanakidhi matakwa ya uhifadhi sahihi na udhibiti wa uchafuzi, kwa lengo la kulinda usalama na ubora wa bidhaa husika wakati wote.

Vilevile, Shirika hufanya ukaguzi katika soko ili kufuatilia ubora na usalama wa bidhaa, kubaini na kuondoa bidhaa ambazo ubora na usalama wake haujahakikiwa, bidhaa zilizoisha muda wa matumizi, vipodozi vyenye viambata sumu na bidhaa ambazo taarifa za kwenye lebo zimeghushiwa kwa lengo la kupotosha watumiaji. Bidhaa zinazobainika kutokukidhi ubora na usalama wakati wa ukaguzi huondolewa katika soko na kuharibiwa kwa kushirikiana na muuzaji ili kulinda afya ya jamii.

TBS inawakumbusha wazalishaji, wasambazaji na wauzaji wa bidhaa za chakula na vipodozi kuendelea kuzingatia taratibu za usajili ili kuhakikisha maeneo ya biashara na bidhaa zinaendelea kukidhi ubora na usalama kwa lengo la kuendelea kulinda afya ya jamii.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia kituo cha huduma kwa wateja kwa namba **0800110827.**

**Imetolewa na:**

Gladness H Kaseka
**Meneja wa Uhusiano na Masoko**


**TBS MAKAO MAKUU**
Shirika la Viwango Tanzania
Barabara ya Sam Nujoma / Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu Na: +255 22 245 0298/ +255 22 245 0206
Nukushi: +255 22 2450959
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: http://www.tbs.go.tz
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya wateja: malalamiko@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS KANDA YA KATI**
Jengo la Kambarage
S. L. P. 2956
DODOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 26 2520310

**TBS KANDA YA ZIWA**
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3
S. L. P. 1814
MWANZA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2505044

**TBS KANDA YA KASKAZINI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 2399
ARUSHA, TANZANIA
Simu Na: +255 27 2520143

**TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S. L. P. 1674
MBEYA, TANZANIA
Simu Na: +255 25 2502848

**TBS KANDA YA KUSINI**
Jengo la MTUWASA
S. L. P. 1396
MTWARA, TANZANIA
Simu Na: +255 23 2334477

**TBS KANDA YA MAGHARIBI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 1276
KIGOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2804023